MMUST PUBLISHING PRESS

Jarida la Kiswahili Sanifu

# Mchango wa Fasihi ya Watoto Katika Ufundishaji wa Stadi za Lugha Katika Shule za Msingi, Mtaala wa Elimu wa Umilisi (CBE) Nchini Kenya

Harriet Ibala*, Tecla Ng'isirei

*Idara ya Isimu Na Lugha, Chuo kikuu cha Moi, Kenya.*

## IKISIRI

Wakati huu ambao Wakenya wamechangamkia Mtaala wa Elimu wa Umilisi (CBE) kama mfumo mpya wa elimu katika shule zote za msingi za umma nchini, ipo haja ya walimu kuibua nyenzo mpya za ufundishaji, ambazo zitamlenga mwanafunzi moja kwa moja. Mojawapo ya nyenzo hizo ni matumizi ya vipera vya Fasihi ya Watoto kufundishia stadi za lugha kwa wanafunzi wa gredi za shule za msingi, yaani kuanzia chekechea hadi gredi ya sita. Fasihi ya watoto ni ile fasihi iliyoandaliwa watoto kama wapokezi na hadhira maalum. Vipera mbalimbali vya Fasihi ya Watoto vinaweza kutumiwa kufundishia wanafunzi katika gredi za shule ya msingi. Vipera hivi vinapotumiwa darasani kufundishia, wanafunzi hufaidi zaidi kwa sababu kupitia kwavyo, maarifa hupokelewa katika mwonoulimwengu wao kama watoto. Yakiongozwa na Nadharia ya Utamaduni Jamii ya Vygotsky (1978), makala haya yanatalii njia mwafaka za kutumia vipera mbalimbali vya fasihi ya watoto kama nyenzo ya ufundishaji wa stadi za lugha. Makala haya vilevile yameweka wazi faida ya fasihi ya watoto kama nyenzo, na kupendekeza njia zinazoweza kutumiwa ili kuepuka udhaifu unaotokana na matumizi ya vipera vya fasihi ya watoto kama nyenzo ya kufundishia. Mbinu za utafiti zifuatazo zimetumiwa kukusanya data ambayo imechanganuliwa na kuwasilishwa kama matokeo; hojaji kwa walimu, mahojiano, na utazamaji darasani, katika masomo ya Kiswahili ya shule za msingi za umma. Matumizi ya Fasihi ya watoto kama nyenzo ya kufundishia stadi za lugha yana umuhimu mkubwa kama vile kukuza stadi za lugha katika muktadha wa kijamii, kukuza uwezo wa kufikiri na tamaduni. Ili kupunguza udhaifu wa kutumia nyenzo hii utafiti umetoa mapendekezo yafuatayo: kabla ya masomo, walimu waandae mazingira ya kuelimisha, kufurahisha na kuvutia. Aidha, wachapishaji, waandishi, na mashirika ya kielimu yaendelee kukuza kazi zinazojikita katika muktadha wa Kiafrika ili kuwavutia watoto zaidi. Pia, Serikali kupitia Wizara ya Elimu pamoja na wadau wa elimu, ianzishe uundaji wa maktaba shuleni. Kando na hayo, wahakikishe kuwa maktaba hizi zimejazwa vitabu vinavyofaa kwa watoto wa umri husika.

## KUHUSU MAKALA

*Maneno Muhimu:*
CBE,
Nyenzo,
Vipera vya Fasihi ya Watoto.

*Historia ya Makala:*
Tarehe ya Kutumwa: 21 Februari 2026
Tarehe ya Kurekebishwa: 23 Machi 2026
Tarehe ya Kukubalika: 27 Machi 2026
Mtandaoni: 8 Mach 2026

## 1. Utangulizi

Mtaala wa Elimu wa Umilisi (CBE) wa somo la Kiswahili, shule ya msingi, umepea stadi za lugha umuhimu mkubwa mno. Jambo hili limesababishwa na ukweli kuwa ni katika kiwango hiki ndipo wanafunzi hupata msingi bora wa uelewa na matumizi ya lugha. Mwanafunzi anayewezeshwa kuelewa stadi za lugha mapema, huweza kuwasiliana vyema, kufikiri kwa kina, na kufaulu kiakademia hata katika viwango vya juu vya elimu, yaani baada ya shule ya msingi. Mtaala wa Elimu wa Umilisi (CBE) nchini Kenya umetilia mkazo ukuzaji wa stadi za lugha kwa wanafunzi wa shule za msingi. Stadi hizi huwawezesha wanafunzi kuwasiliana vyema, kuelewa na kufasiri mambo, na vilevile kujenga msingi bora wa kujifunza na kuendelea kujifunza maishani mwao. Katika Mtaala wa CBE, stadi kama kusikiliza na kuzungumza, kusoma, matumizi ya lugha na kuandika, zinahimizwa kupitia mbinu mbalimbali za kufundishia zinazolenga umilisi. Fasihi ya Watoto, ina jukumu muhimu katika kufanikisha malengo haya. Vipera vya

Fasihi ya Watoto, kama vile hadithi za kubuni, mashairi, nyimbo, na michezo ya kuigiza, vinaweza kutumika kama nyenzo za kufundishia kwa njia ya kuvutia, kuburudisha na kufurahisha. Kando na hayo, Fasihi ya Watoto ina faida tele kwa mwanafunzi wa shule ya msingi. Kwanza kabisa Fasihi ya Watoto hukuza ubunifu na fikra za kina. Watoto wanaposhiriki katika kusoma au kuigiza hadithi, wanajifunza kufikiri kwa njia ya ubunifu na kuelewa maadili mbalimbali. Pia, aina hii

*Mwandishi Mkuu. Barua Pepe: khatenje@yahoo.com

Mhariri: Frida Miruka, Chuo Kikuu cha Masinde Muliro, Kenya.
Nukuu: Ibala H. & Ng'isirei T. (2026). Mchango wa Fasihi ya Watoto Katika Ufundishaji wa Stadi za Lugha Katika Shule za Msingi, Mtaala wa Elimu wa Umilisi (CBE) Nchini Kenya. Jarida la Kiswahili Sanifu 3(1), 24 – 30. https://doi.org/10.61889/jnwcga61.

© 2026 Creative Commons Attribution License (CC BY-NC-SA).

ya fasihi huwezesha wanafunzi kujenga msamiati na uelewa wa lugha kwa kujifunza maneno mapya na jinsi ya kuyatumia katika muktadha sahihi. Fasihi ya Watoto husaidia kukuza maadili na tabia njema na kuelewa kuishi kwa maadili mema kupitia hadithi nyingi za watoto ambazo zina mafunzo ya kimaadili. Isitoshe, Fasihi ya watoto huhamasisha ushirikiano na mawasiliano, huku watoto wakiwezeshwa kushirikiana na wenzao. Hili hutokea kupitia michezo ya kuigiza na majadiliano yanayohusiana na fasihi. Makala haya yanashadidia umuhimu wa tanzu za Fasihi ya Watoto kama nyenzo muhimu ya kufundishia stadi mbalimbali za lugha ya Kiswahili kama somo la lazima katika Mtaala huu wa Elimu wa Umilisi (CBE). Makala yanashinikiza kuwa, vipera vya Fasihi ya Watoto ni nyenzo muhimu ya kufundishia, kwani kupitia vipera hivi, walimu wanaweza kujenga mazingira ya kujifunza yanayovutia, yenye utofauti, na yanayohusiana na maisha halisi ya watoto, hivyo kuchangia katika mafanikio ya Mtaala wa Elimu wa Umilisi (CBE) katika shule za msingi nchini Kenya.

## 2. Uhakiki wa Maandishi

Wataalamu mbalimbali wamezungumzia suala la mbinu za ufundishaji wa stadi za lugha katika viwango mbalimbali vya elimu, kama vile sekondari na vyuo vikuu. Aidha, maandishi mbalimbali yanayohusu Fasihi ya watoto na ufundishaji yameshughulikiwa. Vilevile, tafiti mbalimbali zimefanywa kuhusu fasihi na ufundishaji wa stadi za lugha. Zipo tafiti nyingi zilizohusu mfumo wa awali wa elimu wa Nane Nne Nne (8-4-4) nchini Kenya, na chache mno zinazohusu Mtaala wa Elimu wa Umilisi (CBE). Vilevile zipo tafiti zilizofanywa nje ya nchi ya Kenya, na zile zilizofanya humu nchini. Makala haya yamelenga shule za msingi chini ya Mtaala wa Elimu wa Umilisi (CBE). Pia, kunao utafiti uliofanywa na Ngugi (2017). Utafiti huu unachambua jinsi masuala yanayojitokeza katika jamii yanasawiriwa kupitia Fasihi ya Watoto nchini Kenya. Utafiti huu unatoa mifano ya tini ya Fasihi ya Watoto zinazoshughulikia masuala ya kijamii, na jinsi zinavyoweza kutumika kujenga uelewa na ufahamu kuhusu masuala haya.

Utafiti wa Matundura (2007) unachunguza taswira za uana katika Fasihi ya Kiswahili ya Watoto, ukibainisha jinsi wahusika wa kike na kiume wanasawiriwa na jinsi taswira hizi zinaathiri mtindo wa uandishi. Hizi tafiti zinadhihirisha umuhimu wa Fasihi ya Watoto katika mchakato wa kujifunza, na zinatoa mwanga kuhusu jinsi fasihi hii inaweza kutumika kuboresha stadi za lugha na kueleweshа watoto kuhusu masuala ya kijamii. Aidha, katika Mtaala wa Elimu wa Umilisi (CBE), Fasihi ya Watoto inachangia mno katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za lugha hasa katika gredi za shule za msingi.

Wataalamu mbalimbali wamezungumzia suala la mbinu za ufundishaji wa stadi za lugha katika viwango mbalimbali vya elimu. Aidha, maandishi mbalimbali yanayohusu Fasihi ya Watoto na ufundishaji yameshughulikiwa. Sehemu hii inashughulikia maana ya Fasihi ya Watoto na umuhimu wake katika elimu na Mtaala wa Elimu wa Umilisi (CBE) na malengo yake.

### 2.1. Maana ya Fasihi ya Watoto na Umuhimu Wake katika Elimu

Fasihi ya watoto ni aina ya fasihi inayolenga hadhira ya watoto, hasa wale walio chini ya umri wa miaka kumi na nane. Kwa mujibu wa Ngugi (2019), Fasihi ya Watoto inajumuisha tanzu mbalimbali zikiwemo hadithi fupi, riwaya, mashairi, methali, vitendawili, na ngano. Kazi hizi za fasihi hutumia lugha nyepesi na muundo unaoendana na umri wa watoto, huku wahusika wakuu wakiwa ni watoto au wanyama wanaosawiriwa wakiwa na tabia za kibinadamu. Lengo kuu la Fasihi ya Watoto, kama anavyosema Bakize (2014) huwa ni kufikisha ujumbe wa kimaadili, kijamii, na kitamaduni kwa njia inayovutia na inayoendana na saikolojia ya watoto.

Tafiti mbalimbali zimeonyesha umuhimu wa Fasihi ya Watoto katika ufundishaji wa lugha. Ngugi (2011) anabainisha kuwa Fasihi ya Watoto husaidia katika kukuza ufanisi wa lugha katika shule za msingi nchini Kenya. Nao Faustine & Waziri (2021) wanasisitiza matumizi ya Fasihi ya Kiswahili katika kujifunza kusoma na kuandika.

Wataalamu mbalimbali wameendelea kuzungumzia umuhimu wa Fasihi ya Watoto, na ufundishaji wake katika daraja mbalimbali za elimu nchini Kenya. Hawa ni Ngugi (2019), Bakize (2014), Wamitila (2008; 2010) na Njogu & Chimera (2008). Mawazo yao yanakubaliana na hoja kuwa Fasihi ya Watoto ni muhimu katika elimu nchini Kenya. Wataalamu hawa wanaunga mkono kuwa aina hii ya fasihi ina umuhimu ufuatao;

a) Kukuza Stadi za Lugha: Fasihi ya Watoto inasaidia katika kukuza stadi za kusikiliza na kuzungumza, kusoma, sarufi na kuandika. Kwa mfano, nyimbo na mashairi huchangia katika kujifunza msamiati mpya na miundo ya sentensi.
b) Kufundisha Maadili na Tamaduni: Vipera kama hadithi na methali mara nyingi hubeba maudhui ya maadili kama vile uaminifu, ushirikiano, na heshima. Hii huwasaidia watoto kuelewa na kuthamini tamaduni zao na za wengine.
c) Kukuza Uwezo wa Kufikiri: Kupitia masimulizi ya kifasihi, watoto hufundishwa kufikiri kwa kina, kutatua matatizo, na kuelewa mitazamo mbalimbali. Hii inachangia katika maendeleo yao ya kiakili na kijamii.
d) Kufundisha Stadi za Kusoma na Kuandika: Vipera vya Fasihi ya Watoto, kama vile nyimbo, hutumika kama mbinu ya kufundisha stadi za kusoma na kuandika. Hii inawasaidia watoto kujenga misingi imara ya uandishi na uelewa wa maandishi.

Kutokana na maoni ya wataalamu hawa, Fasihi ya Watoto ni nyenzo muhimu katika elimu, kwani huchangia katika kukuza stadi za lugha, kufundisha maadili, na kukuza uwezo wa kufikiri wa watoto. Vipera vya Fasihi ya Watoto vinapaswa kupewa kipaumbele katika muktadha wa elimu ili kuhakikisha kuwa watoto wanapata wanachohitaji ili kuwakuza katika hali zote za maisha. Mahitaji hayo yanapaswa kutolewa kwa kuzingatia umri wa watoto.

## 2.2. Mtaala wa Elimu wa Umilisi (CBE) na Malengo Yake

Mtaala wa Elimu wa Umilisi (CBE) nchini Kenya ulianzishwa mnamo Desemba 2017 kama sehemu ya mabadiliko katika elimu. Mtaala huu ulilenga kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa kuzingatia umilisi na stadi muhimu za maisha. Kwa mujibu wa Wizara ya Elimu (MoE) 2017, malengo ya Mtaala wa Elimu wa Umilisi (CBE) yameorodheshwa ifuatavyo; Lengo la kwanza ni kukuza Umilisi wa Wanafunzi: Mtaala huu unasisitiza maendeleo ya stadi za maisha kama vile mawasiliano, ushirikiano, ufanisi binafsi, na ufanisi wa kidijitali. Lengo hapa ni kuhakikisha kuwa wanafunzi wanakuwa na uwezo wa kutumia maarifa katika mazingira halisi. Lengo la pili ni kubadilisha mbinu za ufundishaji; Mtaala huu wa Elimu unapendekeza mbinu za ufundishaji zinazozingatia mwanafunzi kama kitovu, kama vile michezo ya kuigiza, utafiti, na miradi, huku walimu wakichukua nafasi ya washauri badala ya wataalamu wa maarifa pekee. Lengo la tatu ni kutathmini maendeleo ya mwanafunzi; Mtaala wa Elimu wa umilisi (CBE) unasisitiza tathmini endelevu kupitia mbinu kama vile mifuko ya kazi, uwasilishaji kwa mdomo, na tathmini za wenzao, badala ya mitihani ya mwisho wa kiwango pekee. Lengo la nne ni kukuza uraia na maadili; Mtaala huu wa Elimu unalenga kukuza maadili ya kijamii na kitaifa, ikiwemo uongozi, ushirikiano, na ufanisi wa kijamii, ili kuandaa wanafunzi kuwa raia na wazalendo bora.

Mtaala wa Elimu wa Umilisi (CBE) unapendekeza njia ya ufundishaji mseto katika masomo mbalimbali na mada tofauti tofauti katika somo. Ili kuwaelewesha wakenya kuhusu ubora wa mtaala huu wa Elimu, Wizara ya Elimu imeeleza faida za ufundishaji mseto ambao unalenga kuunganisha masomo mbalimbali ili kukuza stadi za wanafunzi na kuwaandaa kwa changamoto za ulimwengu wa sasa. Kwa mujibu wa Ngugi (2023), ufundishaji mseto, kama mbinu ya kufundishia stadi za lugha ukitumia vipera vya fasihi ya watoto, una faida zifuatazo;

Kukuza Stadi za Maisha - Ufundishaji mseto husaidia wanafunzi kukuza stadi muhimu za maisha, kama vile ushirikiano, kupitia kazi za makundi na miradi ya pamoja. Uongozi - yaani mwanafunzi anaweza kuchukua majukumu ya uongozi katika shughuli za darasani. Uwasilishaji - mwanafunzi anaweza kuwasilisha mawazo mbele ya wenzake. Utatuzi wa matatizo - unaweza kufanywa na wanafunzi kwa kutumia mbinu za ubunifu katika kukabiliana na changamoto.

Kukuza ufanisi wa kiusomi na kisarufi - Mbinu hii inawawezesha wanafunzi kuelewa muktadha wa matumizi ya lugha, kwa kuunganisha masomo kama Kiswahili na sayansi. Aidha, mbinu hii huwezesha ujenzi wa msamiati kupitia matumizi ya maneno katika muktadha halisi. Pia, hukuza ufanisi wa kisarufi kwa kutumia mifano halisi kutoka kwa masomo mbalimbali.

Kukuza uelewa wa muktadha wa kitamaduni na mazingira - Ufundishaji mseto unahimiza kuelewa na kuthamini tamaduni mbalimbali kupitia masomo ya sanaa na historia na kuchukua hatua za uhifadhi wa mazingira kupitia masomo ya sayansi na kilimo.

Kukuza Ufanisi wa Kidijitali - Mbinu hii inahimiza matumizi ya teknolojia katika kujifunza kupitia matumizi ya vifaa vya kidijitali katika masomo mbalimbali. Inahimiza vilevile uwezo wa kutafuta na kutumia taarifa mtandaoni kupitia utafiti na miradi ya mtandaoni.

Kukuza Ufanisi wa Kijamii na Hisia - Ufundishaji mseto unahimiza kuelewa na kuthamini utofauti wa kijamii kupitia masomo ya sanaa na historia. Hukuza hisia za usawa na haki kupitia masomo ya uraia na maadili.

Kwa hivyo, ufundishaji mseto katika Mtaala wa Elimu wa Umilisi (CBE) unalenga kuwaandaa wanafunzi kuwa raia bora na wenye ufanisi katika jamii. Kwa kuunganisha masomo mbalimbali, wanafunzi wanapata uelewa wa kina na wa muktadha, unaowawezesha kutumia stadi zao katika maisha halisi.

Misingi ya kinadharia: Nadharia ya Utamaduni wa jamii ya Vygotsky (1978) katika Muktadha wa Ufundishaji wa Stadi za Lugha

Makala haya yameongozwa na mihimili ya Nadharia ya Utamaduni Jamii, ya Vygotsky (1978). Nadharia hii inaafiki kuwa fasihi ni nyenzo bora ya kufundishia stadi za lugha. Vilevile, hii ni nadharia inayosisitiza kuwa maendeleo ya kiakili ya binadamu yanategemea mwingiliano wa kijamii na muktadha wa kitamaduni. Katika muktadha wa ufundishaji wa stadi za lugha, nadharia hii inatoa mwanga kuhusu jinsi walimu wanaweza kutumia Fasihi ya Watoto kama nyenzo muhimu katika kukuza stadi za lugha kwa wanafunzi wa shule za msingi, chini ya Mtaala wa Elimu wa Umilisi (CBE). Kupitia misingi mitatu, Vygotsky anashinikiza umuhimu wa Nadharia ya Utamaduni Jamii katika ufundishaji wa stadi za lugha. Misingi hii ni kama ifuatavyo;

a) Maendeleo ya kiakili kama mchakato wa kijamii: Vygotsky (1978) alisisitiza kuwa maendeleo ya kiakili yanatokea kupitia mwingiliano wa kijamii. Kwa mfano, mtoto anaposhirikiana na mzazi au mlezi katika shughuli za kila siku, anajifunza na kuimarisha stadi za lugha. Hii ina maana kuwa lugha ni chombo cha mawasiliano kinachochochea na kuimarisha mchakato wa kujifunza.
b) Mazingira na maendeleo ya mtoto: Katika msingi huu, Vygotsky (1978) anarejelea umbali kati ya kile mtoto anaweza kufanya peke yake na anachoweza kufanya kwa msaada wa mwingine mwenye ujuzi zaidi. Katika muktadha wa ufundishaji wa fasihi ya watoto, walimu wanaweza kutumia msingi huu kwa kutoa msaada unaohitajika ili wanafunzi wafikie kiwango cha juu cha ufanisi katika stadi za lugha.
c) Madhumuni ya kazi ya utamaduni wa jamii: Vygotsky (1978) alieleza kuwa kazi za utamaduni wa jamii, kama vile methali, hadithi, na nyimbo, ni zana zinazotumiwa na jamii katika kufundisha na kuhamasisha stadi za lugha. Kwa kutumia kazi hizi, walimu wanaweza kuwasaidia wanafunzi

kuelewa na kutumia lugha katika muktadha wa kijamii na kitamaduni.

Nadharia ya Utamaduni jamii inahusiana na kuchangia ufundishaji wa stadi za lugha katika shule za msingi, Mtaala wa Elimu wa Umilisi (CBE), kwa njia mbalimbali, kupitia kwa mihimili yake. Kwanza kabisa kupitia Ushirikiano wa kijamii katika kujifunza. Hapa, walimu wanapaswa kuhamasisha wanafunzi kushirikiana katika shughuli za kujifunza, kama vile kujadili hadithi, kuimba nyimbo, na kuigiza michezo. Hii inawawezesha wanafunzi kujifunza kutoka kwa wenzao na kuimarisha stadi zao za lugha. Pili, Nadharia ya Utamaduni jamii katika muktadha wa kujifunza lugha inasisitiza umuhimu wa mazingira ya kijamii na kitamaduni katika mchakato wa kujifunza. Inatambua kwamba lugha ni sehemu muhimu ya utamaduni na kujifunza lugha kunahusisha pia kujifunza tamaduni zinazohusiana nayo. Hii inamaanisha kwamba matumizi ya Fasihi ya Watoto kama nyenzo ya kufundishia stadi za lugha yanapaswa kuzingatia vipengele vya kitamaduni ili kuwe na ufanisi zaidi. Kwa kutumia zana za utamaduni katika kufundisha, walimu wanapaswa kutumia methali, hadithi, na nyimbo kama zana za kufundishia. Kwa mfano, hadithi za Kiswahili zinazohusiana na maadili na tamaduni za Kiafrika zinaweza kutumika kuwafundisha wanafunzi msamiati mpya na matumizi sahihi ya lugha. Mhimili wa tatu unashinikiza kufundisha kupitia utoaji wa msaada unaohitajika. Kupitia njia hii, walimu wanapaswa kutoa msaada unaohitajika kwa wanafunzi ili wafikie kiwango cha juu cha ufanisi katika stadi za lugha. Hii inaweza kujumuisha kutoa mifano, kuuliza maswali ya kufikirisha, na kutoa mrejesho unaojenga.

Nadharia ya Utamaduni jamii ya Vygotsky (1978) inatoa msingi madhubuti wa kutumia Fasihi ya Watoto kama nyenzo muhimu katika ufundishaji wa stadi za lugha. Kwa kuzingatia misingi ya nadharia hii, walimu wanaweza kuboresha mbinu zao za ufundishaji na kuwasaidia wanafunzi kufikia ufanisi katika stadi za lugha.

Wapo wataalamu wanaoshikilia kuwa, tanzu za Fasihi ya Watoto zikiwemo hadithi, methali, na nyimbo, zinatoa mifano halisi ya matumizi ya lugha katika muktadha wa kijamii. Wataalamu hawa ni Faustine & Waziri (2021). Wao wanasema kuwa, kwa kutumia vipera hivi, wanafunzi wanapata nafasi ya kujifunza maneno, msamiati, na miundo ya sentensi inayotumiwa katika mazungumzo ya kila siku. Hii inawawezesha kuelewa na kutumia lugha katika muktadha halisi, hivyo kuboresha ufanisi wao katika stadi za kusikiliza na kuzungumza, sarufi, kusoma na kuandika. Kwa hivyo, kutumia Fasihi ya Watoto kama nyenzo ya kufundishia stadi za lugha sio tu kuboresha ufanisi wa kujifunza, bali pia kunahakikisha kwamba wanafunzi wanajifunza lugha katika muktadha wake halisi wa kitamaduni. Nadharia ya utamaduni jamii inasisitiza kuwa kujifunza lugha ni mchakato unaohusisha mazingira ya kijamii na kitamaduni ambayo mtu anapitia. Katika muktadha wa Mtaala wa Elimu wa Umilisi (CBE) nchini Kenya, matumizi ya vipera vya Fasihi ya Watoto kama nyenzo ya kufundishia stadi za lugha yanahusiana sana na Nadharia ya Utamaduni jamii, kwa njia zifuatazo;

a) Kukuza uelewa wa tamaduni na maadili: Vipera vya Fasihi ya watoto, kama vile hadithi, methali, na nyimbo, hubeba maudhui na maadili ya kijamii. Kwa kutumia vipera hivi, wanafunzi wanajifunza kuhusu tamaduni zao na za wengine, hivyo kukuza mshikamano wa kitaifa na kuelewa utofauti wa kijamii. Ngugi (2023) anabainisha kuwa Fasihi ya Watoto inaweza kuchangia katika uendelezaji na uimarishaji wa mshikamano wa kitaifa.
b) Kukuza stadi za lugha katika muktadha wa kijamii: Matumizi ya Fasihi ya Watoto hutoa mifano halisi ya matumizi ya lugha katika muktadha wa kijamii. Hii inawawezesha wanafunzi kuelewa na kutumia lugha katika mazungumzo ya kila siku, hivyo kuboresha stadi zao za kusikiliza na kuzungumza, sarufi, kusoma na kuandika. Faustine & Waziri (2021) wanasema kuwa nyimbo za Kiswahili katika fasihi ya watoto huchangia sana katika kujifunza kusoma na kuandika.
c) Kufundisha maadili na tamaduni: Hadithi na methali kama vipera vya Fasihi ya Watoto mara nyingi hubeba maudhui ya maadili na utamaduni. Kwa mfano, Ngugi (2011) alichambua Fasihi ya Watoto katika shule za msingi nchini Kenya na kugundua kuwa matumizi ya Fasihi ya Watoto yanasaidia katika kujenga utamaduni wa usomaji na kuelewa maadili ya kijamii.

Nadharia ya Utamaduni jamii inavyohusiana na matumizi ya Fasihi ya Watoto katika ufundishaji wa stadi za lugha chini ya Mtaala wa Elimu wa Umilisi (CBE) inadhihirika katika jinsi vipera hivi vinavyosaidia wanafunzi kuelewa na kutumia lugha katika muktadha wa kijamii, huku wakijifunza maadili na tamaduni zinazohusiana. Fasihi ya Watoto ni nyenzo muhimu katika kujenga maarifa na kukuza stadi za lugha miongoni mwa watoto. Inapochanganuliwa, Fasihi ya Watoto inajumuisha hadithi, mashairi, methali, na nyimbo zinazowasilisha maudhui mbalimbali zinazohusiana na maisha ya kila siku, tamaduni, na maadili. Fasihi ya Watoto ni chombo muhimu cha kujenga maarifa na kukuza stadi za lugha. Inapochangia katika uelewa wa tamaduni, maadili, na kuboresha uwezo wa lugha, fasihi hii inawaandaa watoto kuwa raia wenye ufanisi katika jamii.

## 3. Mbinu za Utafiti

Mbinu mbalimbali zilitumiwa katika kukusanya data ambayo ilipangwa, kuchanganuliwa na kuwasilishwa kama matokeo, kuhusu matumizi ya vipera vya fasihi ya watoto kama nyenzo ya kufundishia stadi za lugha katika shule za msingi, chini ya Mtaala wa Elimu wa Umilisi (CBE), nchini Kenya. Mbinu hizi zilijumuisha hojaji kwa walimu, mahojiano, na utazamaji darasani wa walimu katika masomo yao ya Kiswahili katika shule za msingi za umma. Sampuli iliyotumiwa ilijumuisha shule nane za umma ambazo ziliteuliwa kimakusudi mjini Eldoret. Walimu watatu wa somo la Kiswahili, gredi za msingi (yaani gredi ya kwanza hadi ya sita) waliteuliwa kutoka

kila shule. Jumla, walimu ishirini na nne walishiriki katika utafiti huu.

## 4. Mchango wa fasihi ya watoto katika ufundishaji wa stadi za lugha

Kutokana na shughuli za kutazama ufundishaji darasani, majibu ya hojaji na mahojiano na walimu, ilidhihirika wazi kuwa katika muktadha wa Mtaala wa Elimu wa Umilisi (CBE) nchini Kenya, vipera vya Fasihi ya Watoto ni nyenzo yenye uwezo mkubwa wa kusaidia kukuza stadi mbalimbali za lugha, kama vile kusikiliza na kuzungumza, matumizi ya lugha, kusoma na kuandika. Makala haya yanapendekeza kuwa vipera mbalimbali vya Fasihi ya watoto vitumiwe na walimu darasani, kama nyenzo ya kufundishia stadi za lugha. Matokeo ya utafiti wa sasa yanaunga mkono yale ya utafiti wa Faustine & Waziri (2021) ambao unabainisha kwamba vipera vya Fasihi ya Watoto, hasa nyimbo, zinaweza kutumika kama mbinu kuu ya kufundishia stadi za lugha. Utafiti huu uliofanyika Tanzania ulionyesha kuwa nyimbo za Kiswahili kama vipera vya Fasihi ya Watoto huchangia sana katika kujifunza kusoma na kuandika. Mikakati ifuatayo ilipendekezwa na walimu kama inayotoa mchango mkubwa na inayoweza kusaidia walimu kutumia vipera vya Fasihi ya Watoto kwa mafanikio zaidi:

Walimu wa somo la Kiswahili katika shule za msingi walipendekeza matumizi ya mbinu shirikishi darasani, yaani, mbinu kama maigizo ya hadithi, maigizo ya methali, kusoma kwa sauti kwa pamoja na kuimba nyimbo za lugha ya Kiswahili zenye maudhui ya kijamii. Mbinu hizi zilionekana kama zilizo na uwezo wa kuchochea wanafunzi kushiriki masomoni kikamilifu, kukuza uelewa wa lugha na kuboresha kumbukumbu. Baadhi ya walimu wanatumia mbinu hii na wameweza kufaulisha ufundishaji wa stadi mbalimbali za lugha.

Kuna mchango mkubwa wa vipera vya Fasihi ya watoto walimu wanapotumia uchanganuzi wa maudhui ya fasihi wanapofundisha. Walimu wengi, kupitia hojaji na mahojiano walipendekeza uchambuzi wa maudhui ya hadithi au mashairi kwa kuhusisha na maisha halisi ya wanafunzi. Vilevile, walipendekeza matumizi ya maswali ya kufikirisha kuhusu wahusika na matukio ya kazi za fasihi. Njia hii inasaidia wanafunzi kujifunza msamiati mpya na kuelewa matumizi ya lugha katika muktadha. Kupitia utazamaji wa ufundishaji darasani, mtafiti alithibitisha kuwa hii ni njia ya ufundishaji iliyokuwa na mchango mkubwa katika kufaulisha shughuli ya ufundishaji darasani.

Mazingira ya ufundishaji ambayo yanafurahisha vilevile yalionekana kuwa na mchango mzuri katika kufaulisha ufundishaji wa stadi darasani. Pamoja na mazingira, walimu walipendekeza uanzishaji wa maktaba ya darasa yenye vitabu vya fasihi ya watoto. Vilevile, walitoa maoni kuwa wanaweza kuhimiza wanafunzi kuwa na usomaji wa kujitegemea na kuandaa vipindi vya "hadithi ya wiki". Walimu walihimiza uhusishaji wa wazazi na jamii katika kusimulia hadithi au kutoa vitabu kwa ajili ya wanafunzi/watoto kuvitumia shuleni na nyumbani. Hii ni njia ambayo inawawezesha wanafunzi kusoma katika mazingira faafu na hivyo kutoa mchango mkubwa katika ufundishaji wa stadi za lugha.

Baadhi ya walimu waliojibu hojaji na kushiriki katika mahojiano walitoa mapendekezo yao wenyewe kutumia video, sauti, au programu za Fasihi ya Watoto kwa lugha ya Kiswahili wakiwa darasani wakati wa kufundisha stadi za lugha. Vilevile walipendekeza kuwaruhusu wanafunzi kurekodi hadithi zao au mashairi kwa kutumia simu tamba, au redio ya shule, kisha kazi hizi zisikilizwe baada ya mafundisho ya darasani. Vyombo vya kiteknolojia vilitumiwa katika baadhi ya madarasa ambamo mtafiti aliingia kutazama masomo ya Kiswahili. Ilidhihirika wazo kuwa vyombo vya kiteknolojia vinatoa mchango mkubwa katika ufundishaji darasani.

Kila mwanafunzi anatoka katika jamii iliyo na utamaduni wake mahsusi, ambao unastahili kuimarishwa vilivyo shuleni. Umuhimu wa kuchagua kazi za fasihi zenye muktadha wa Kiafrika na kuzingatia mila na desturi zinazowiana na mazingira ya mwanafunzi ni mchango mkubwa katika makuzi ya wanafunzi. Hali hii ilidhihirika darasani kupitia utazamaji wa masomo ya Kiswahili. Walimu walitumia methali, nahau na semi za kiasili kama nyenzo za mafunzo.

Kupitia hojaji na mahojiano, majibu ya walimu yalipendekeza kuwa mikakati shirikishi, ya ubunifu, na inayozingatia mazingira ya wanafunzi ni njia bora ya kutumia Fasihi ya Watoto katika kufundisha stadi za lugha. Walidahili kuwa walimu, wazazi na watunga sera wanapaswa kushirikiana kuhakikisha mazingira yanawezesha utekelezaji wa mikakati hii kwa ufanisi chini ya Mtaala wa Elimu wa Umilisi (CBE). Hii itatoa mchango mkubwa katika ufundishaji wa stadi darasani.

## 5. Changamoto za kutumia tanzu za Fasihi ya Watoto kama Nyenzo ya Kufundishia Stadi za Lugha chini ya Mtaala wa Elimu wa CBE nchini Kenya

Kwa mujibu wa walimu walioshiriki katika utafiti huu, Fasihi ya Watoto ni nyenzo muhimu katika kufundisha na kukuza stadi za lugha miongoni mwa wanafunzi wa shule za msingi. Walimu hawa wanadahili kuwa matumizi yake kama nyenzo ya kufundishia chini ya Mtaala wa Elimu wa Umilisi (CBE) nchini Kenya yanakumbana na changamoto mbalimbali. Kupitia utazamaji darasani wa walimu waliokuwa wanafundisha masomo ya Kiswahili, hojaji zilizojazwa, pamoja na mahojiano, changamoto zifuatazo zilidhihirika wazi kama zinazokabili matumizi ya fasihi ya watoto katika ufundishaji wa stadi za lugha;

a) Upungufu wa vifaa vya Fasihi ya Watoto; shule nyingi, hasa za umma, hazina nakala za kutosha za vitabu vya fasihi ya watoto, pamoja na vifaa vinavyoandamana na utendaji wa vipera vya fasihi ya watoto kama vile maleba na ala za muziki. Aidha, baadhi ya vitabu na ala zinazopatikana katika shule nyingi hazijazingatia mazingira halisi ya mtoto wa Kiafrika au Mkenya.
b) Ukosefu wa mafunzo maalum kwa walimu; walimu wengi hawajapokea mafunzo ya kina kuhusu jinsi

ya kutumia tanzu za Fasihi ya Watoto kama nyenzo ya kufundishia stadi za lugha. Vilevile, walimu hawajapata masomo ya ziada yanayowawezesha kufaragua mbinu mpya za ufundishaji.

c) Mwitikio hafifu kutoka kwa wanafunzi; baadhi ya wanafunzi wanapokea fasihi kama kazi ngumu au ya kuchosha, hasa pale inapowasilishwa kwa njia isiyovutia. Kwa sababu hii, baadhi ya wanafunzi hawapendelei kufundishwa kwa kutumia uwasilishaji wa vipera mbalimbali vya Fasihi ya Watoto, kwani sio watoto wote wanaopendelea kushiriki vipera vya Fasihi ya Watoto.

d) Kukosekana kwa muktadha wa kitamaduni; Baadhi ya vipera vya Fasihi ya Watoto vinaiga sana fasihi ya kimagharibi na kupuuza utamaduni wa Kiafrika. Hivyo, vipera hivi huwa na ugeni fulani miongoni mwa wanafunzi, ugeni unaoweza kutinga ujifunzaji.

e) Ukosefu wa mwelekeo katika Mtaala; Ingawa Mtaala wa Elimu wa Umilisi (CBE) unasisitiza matumizi ya nyenzo mbalimbali za ufundishaji, haujaweka wazi namna ya kuchanganya Fasihi ya Watoto katika ufundishaji wa lugha.

## 6. Hitimisho

Tanzu za fasihi ya watoto ni nyenzo muhimu katika Mtaala wa Elimu wa Umilisi (CBE). Tanzu hizi zinachangia katika kukuza stadi za lugha, maadili, na ufahamu wa kitamaduni kwa njia inayovutia na inayolenga maendeleo ya mwanafunzi kwa ujumla. Walimu wanapaswa kupewa mafunzo na rasilimali stahiki ili kutumia ipasavyo tanzu hizi katika muktadha wa elimu ya msingi katika shule za viwango hivyo. Ufundishaji katika shule za msingi kwa kutumia vipera vya Fasihi ya Watoto kama nyenzo ya kufundishia unaingiliana moja kwa moja na mahitaji ya Mtaala wa Elimu wa Umilisi (CBE) kwani mfumo huu unasisitiza umuhimu wa maendeleo jumulishi kwa mwanafunzi (holistic development). Ufundishaji jumulishi huhusisha mbinu ya ufundishaji inayolenga kukuza mwanafunzi kikamilifu, yaani kiakili, kihisia, kijamii, na kiroho. Katika muktadha wa Kiswahili, ujifunzaji jumulishi unahusisha mbinu shirikishi kama vile majadiliano, uimbaji wa nyimbo na mashairi, michezo ya kuigiza, na uandishi wa hadithi na usimuliaji wake, ili kukuza stadi za lugha na pia kuwaandaa wanafunzi kuwa raia bora katika jamii. Matumizi ya Fasihi ya Watoto na vipera vyake kama mbinu ya kufundisha itawezesha walimu kutimiza malengo yao ya ufundishaji, huku wanafunzi wakieleweshwa vilivyo yale wanayofundishwa. Wakuza mitaala vilevile watakuwa na wakati mwepesi wanapotimiza malengo yao waliopangia mtaala wa elimu katika gredi za msingi za Mtaala wa Elimu wa Umilisi (CBE).

## 7. Mapendekezo

Fasihi ya Watoto ni chombo muhimu katika kujenga maarifa na kukuza stadi za lugha. Ingawa kuna changamoto katika matumizi yake kama nyenzo ya kufundishia, utafiti huu, kupitia matokeo yake, umeonyesha mwanya unaotakiwa kuzibwa. Mapendekezo yafuatayo yanalenga kuboresha ufanisi katika kufundisha stadi za lugha miongoni mwa wanafunzi wa shule za msingi chini ya Mtaala wa Elimu wa Umilisi CBE nchini Kenya.

a) Ili kuendeleza Fasihi ya Watoto wa Kiafrika, wachapishaji, waandishi, na mashirika ya kielimu yaendelee kukuza kazi zinazojikita katika muktadha wa Kiafrika ili kuwavutia watoto zaidi.

b) Kupitia Wizara ya Elimu (MoE) na Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya (KICD) serikali itoe mafunzo ya mara kwa mara kuhusu njia bora za kutumia Fasihi ya Watoto katika ufundishaji kwa walimu.

c) Walimu washauriwe kutumia mbinu shirikishi na ubunifu katika kufundisha, kwa kutumia maigizo, uigizaji wa hadithi, nyimbo, na mashairi kwa njia za kiubunifu ili kuongeza mvuto na ushiriki wa wanafunzi.

d) Serikali kupitia Wizara ya Elimu pamoja na wadau wa elimu, ianzishe uundaji wa maktaba shuleni. Kando na hayo, wahakikishe kuwa maktaba hizi zimejazwa vitabu vinavyofaa kwa watoto wa umri husika.

e) Jamii, wazazi na walimu wahusishwe katika kuhimiza watoto kusoma fasihi kwa ajili ya kujifurahisha na kujifunza ili ushirikiano huu uwawezeshe watoto kujifunza fasihi nyumbani na shuleni ili hali hii isaidie kufaulisha ujifunzaji darasani kupitia vipera mbalimbali vya fasihi.

## Marejeleo


Bakize, L. (2014). Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili ya Watoto nchini Tanzania na Kenya: Mkabala Linganishi. Academia.edu.

Faustine, S., & Waziri, S. (2021). Fasihi ya Watoto ya Kiswahili: Mbinu ya Kufundishia na Kujifunza Kusoma na Kuandika. Jarida la Chama cha Lugha na Fasihi ya Kiswahili Tanzania (CHALUFAKITA). Eissn: 2591-7013 print ISSN: 2665-0789

Lyimo, E. B. (2016). Dhima ya Nathari katika Fasihi ya Watoto: Mifano kutoka Tanzania. Kioo cha Lugha. 15(1)

Lyimo, E. B. (2016). Dhima na Mianzo na Miisho katika Nathari za Kiswahili za Fasihi ya Watoto: Mifano kutoka Riwaya na Hadithi za Kiswahili za Watoto nchini Tanzania. Kioo cha Lugha, 15(1).

Matundura,E.S.(2007). Taswira Dumifu za Uana katika Fasihi ya Kiswahili ya Watoto. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili katika Isimu na Lugha. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Ngugi, P. M. Y. (2019). Fasihi ya Watoto katika Ufundishaji wa Kiswahili katika Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki. KAKAMA

Ngugi, P. M. (2011). Ufundishaji wa Fasihi ya Watoto katika Shule za Msingi Nchini Kenya. Kioo cha Lugha. 9(1)

Ngugi, D.PM.N(2017) Usawiri wa Masuala Ibuka katikaFasihi ya Watoto: Mfano kutoka Kenya Mulika Journal 35(1) http://ir-library.ku.ac.ke/handle/123456789/26475

Ngugi, P. M. Y. (2023). Mitaala ya Kiswahili Katika Elimu na Utaifa: Nafasi ya Fasihi ya Watoto Katika Uendelezaji na Uimarishaji wa Mshikamano wa Kitaifa. Twaweza Communications.

Njogu, K., & Chimera, R. (2008). Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Vygotsky, L. S. (1978). Mind in Society: The Development of Higher Psychological Processes. Harvard University Press.

Wamitila, K. (2008). Ufundishaji wa Fasihi ya Watoto. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. (2010). Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi. Nairobi: Vide - Mua Publisher.